Jinsi ya Kuanza Changamoto ya Biblia kwa Mtu Mmoja

-Na Mch. Marek P. Zabriskie, Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Christ Church Greenwich (Connecticut) Mwanzilishi wa Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia
www.thecenterforbiblicalstudies.org.

Rafiki Mpendwa,

Tunakukaribisha wewe katika Changamoto ya Biblia. Tumefurahishwa kwamba umependa kusoma maneno ya Mungu yaletayo mabadiliko maishani. Itabadirisha na kustawisha maisha yako. Hapa kuna baadhi ya vitu ambavyo tunakuhamasisha wewe kusoma na kuzingatia kabla ya kuanza.

Wazo la mwanzo kuhusu kuisoma Biblia

Unaweza kuanza Changamoto ya Biblia muda wowote wa mwaka ambao utautaka.
Tunakuhimiza kusoma sehemu ya Biblia kila siku
Tunapendekeza kwamba ujipe mwenyewe mwaka kuisoma Biblia
Baadhi ya watu wanajaribu kusoma Biblia kwa siku 90, lakini mfumo wa muda mfupi unaweza kukatisha tamaa. Biblia ina ujumbe mzito sana , na tunapendekeza kwamba chukua muda wa kutosha kuruhusu maneno ya Mungu kupenyeza moyoni mwako, kukumbuka na kuzama rohoni.

Kama unahitaji zaidi ya mwaka kusoma Biblia yote, tunakuunga mkono kwa kukusogeza katika hatua itakayofanya kazi vizuri kwako.
Tovuti yetu *thecenterforbiblicalstudies.org*, inatoa njia nyingi kukusaidia wewe.

Tafsiri ipi ya Biblia ninayolazimika kusoma?

Tunahimiza washiriki kusoma “The New Oxford” tafsiri yenye ufafanuzi ya Biblia. Ni nzuri sana , tafsiri inayosomwa sana yenye

msaada rejea. Tafsiri ya Biblia ya “The New International” na tafsiri ya “Common English” ni tafsiri nyingine nzuri. Kuna nyingi nyingine tafsiri nzuri za Biblia. Kama utapenda kusoma moja tofauti, tafadhari jisikie huru kufanya hivyo. Chukulia akilini kwamba kutumia tafsiri ya mfalme James kusoma Biblia kwa mara ya kwanza inaweza kuwa ngumu.

Hatamu ya nguvu ya teknolojia. Washiriki wengi wa Changamoto ya Biblia wanasoma Biblia wakitumia *ipad* zao, *iphone*, *kindle* au *Nook* au wanasikiliza Biblia kwenye CDs. Tafsiri ya Biblia ya NIV tayari inapatikana kwenye CD. Baadhi ya washiriki wa Changamoto ya Biblia wamechagua kutumia siku-365- Biblia. Tafadhari nukuu, hatahivyo kwamba hizi siku za kuisoma Biblia mara zote huepuka baadhi ya masimulizi ya Biblia.

Washiriki wengi katika Changamoto ya Biblia husoma Biblia yote. Hiki ndicho tunachoshauri. Kama zoezi hili linaonyesha kukatisha tamaa, hivyo tunakusisitiza wewe kwa 1) Soma Agano Jipya au 2) Soma moja kati ya Injiri au 3) Soma kitabu

cha Matendo 4) Soma Zaburi(kitabu cha Zaburi) na pambana/gusa changamoto kubwa baadae.
Waamerika wengi hufanya mwaka mpya ulioimara/thabiti. Mara nyingi kwa kawaida uimara wa mwaka mpya kwa Amerika ni kupunguza uzito. Kitu cha pili kwa kawaida kuimarishwa ni kufanya mazoezi zaidi mara kwa mara. Ndani ya siku sita Waamerika wengi huondoka uthabiti wao. Wanasaikolojia wanasema kwamba hii hutokea kwa sababu watu wafanyao uthabiti hawana hata mmoja wa kuhimiri kuwawajibisha. Hivyo ni muhimu kutoa msaada endelevu na kushikilia uimara wa wau, hasa hasa kupita miezi mitatu ya Changamoto ya Biblia. Wale wanaofanikiwa kwa siku 90 huelekea kufikia malengo yao.

Imarisha timu na kuufikia msaada wa kusoma biblia

Njia mojawapo ya kujipa mwenyewe uwajibikaji kwa kusoma maneno ya Mungu na kukusaidia wewe kuisoma Biblia ni kuanzisha kikundi ndani ya kanisa lako au jamii. Kwa kushirikiana katika changamoto ya

biblia pamoja mnaweza kujisaidia mmoja na mwingine katika kujisomea, kuuliza maswali kuhusu biblia, kujadili nini mmesoma na kushiriki kivipi kusoma maneno ya Mungu yamebadirisha maisha yako.

Kama hutotaka kuanzisha kikundi chako, tuna kusisitiza kutafuta kikundi kanisani kwako au jamii yako au zingaia kusoma Biblia pamoja na rafiki au kikundi cha marafiki. Ni muhimu kushirkisha kile unachokisoma , uliza maswali kuhusu Biblia na shirikisha kivipi kusoma maneno ya Mungu kumebadirisha maisha yako.

Tunaita madarasa yetu ya msaada “maongezi ya wenye akili kuhusu Biblia” baadhi huita kikundi chao cha msaada “chama cha kitabu kizuri” na majina mengine. Makundi haya yatatoa msaada kwa wanafunzi wanaosoma Biblia, zaidi katika kipindi cha siku 90 za mwanzo za kujisomea pale wanafunzi wa usomaji wanapopita katika maandiko ya Waebrania na wakishindana na masimulizi ya vurugu, maamuzi ya ghadhabu kuwa tabia ya Mungu, wanawake kutendewa kimaskini na uhalisia wa ajabu kama vile maisha ya watu kufikia miaka 920. Kama mwanafunzi wa usomaji atakuwa tayari kufanya kazi kupitia sehemu ngumu, mafanikio yatawezekana.

Unaweza kuuliza kanisa lako kuona kama unaweza kuweka muhtasari katika kijarida cha parishi kwamba unaanzisha kikundi kujiunga na Changamoto ya Biblia kuisoma Biblia yote pamoja. Karibisha wengine kuungana nawe na kuja pamoja kwa kawaida kujadili masomo yenu, maswali, kujifunza na kivipi imebadirisha maisha yako. Tafadhari angalia “kivipi waumini watashiriki”, kwa msaada wa maoni, kama una matakwa yakuanzisha kikundi katika kanisa kujiunga na Changamotoo ya Biblia.

Kama utaunda kundi kusoma Biblia yote pamoja, tunakuhamasisha kuandaa sherehe ya kuwakusanya au chakula kufurahia utimilifu wako wa kiroho.

Ruhusu kituo cha kujifunza Biblia kukusaidia

Kama una maswali kuhusu kile unachokisoma, tunakusisitiza kutuandikia barua pepe katika kituo cha kujifunza Bibli na tutajitahidi kujibu papo hapo. Tunakusisitiza kuwa na furaha na kutafuta amani ya kiroho na shangwe ambayo Mungu anaitaka kwako katika usomaji wako wa kila siku. Malengo yetu ya mwisho ni kukufanya wewe ugundue hekima ya Mungu katika usomaji wako wa kila siku wa Biblia na kutengeneza mazoezi ya kiroho ya maisha ya kujisomea Biblia kila siku ili kwamba Mungu aweze kuongea nawe kwa utulivu na kwa upekee na akuongoze katika maisha yako ya kila siku.

Maisha baada ya Changamoto ya Biblia

Kama umejikuta umesoma Biblia yote na umekuwa sehemu ya Changamoto ya Biblia kuweza kubarikiwa katika maisha yako, hivyo tunakusisitiza sana kushiriki baraka. Karibisha marafiki kadhaa au wanajumuiya wa familia kushiriki katika Changamoto ya Biblia.

Wale waliofanikiwa kusoma Biblia yote wanaweza kutamani kusoma Biblia tena wakitumia tafsiri tofauti.
Tunasisitiza sana washiriki kufanya usomaji wa Biblia kila siku ni zoezi la muhimu la kiroho mpaka mwisho wa maisha yao. Biblia ni kitabu cha thamani kilichowekwa wakfu katika kipindi cha maisha kukisoma na kukirudia kusoma. Ni chemchemi ya hekima isiyoisha ambayo itatawaza baraka juu yetu katika siku zote za maisha yetu, kwahiyo usomaji mmoja wa Biblia ni kitu cha kufurahia kupata kukitengeneza.

Kuna wale kama Rais John Adam, Rais wa pili wa Marekani aliefanya zoezi la kupitia kuisoma Biblia kila mwaka wakati wa maisha yake ya utu uzima na kuguswa sana na baraka kwa kufanya hivyo. Tunapigania sana zoezi hili.
Baada ya kupitia kuisoma Biblia mara ya kwanza utakuwa na uwezo zaidi mno kusaidia kuhamasisha na kusaisia wengine katika kuisoma Biblia yote. Tunakuhamasisha kuwa kama mhamasishaji na msimamizi kwa wengine kufanya hili.

Kwa mara nyingine tunakuhamasisha kwamba umekubari kushiriki katika Changamoto ya Biblia. Mwenyezi Mungu akubariki kwa wingi kwa kufanya maamuzi haya na akusaidie kuheshimu maamuzi yako ya kusoma maneno ya Mungu.

©